JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# MUHTASARI WA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA 30 JUNI 2013 KWA VYOMBO VYA HABARI

**Taarifa ya mambo muhimu yaliyopo kwenye Ripoti hizo na kama zilivyowasilishwa Bungeni, Tarehe 7 Mei, 2014**

**Ndugu Wanahabari,**

1. Kwa heshima kubwa naomba kutoa kwenu na kwa wananchi muhtasari wa masuala ya msingi yaliyojitokeza katika ripoti zangu za ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2013.

## Utangulizi

2. Katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2013, nilifanya ukaguzi katika Halmashauri 140, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali 117, Mashirika na Taasisi za Umma 93, jumla ya Miradi ya Wafadhili 611 ikijumuisha; Miradi ya Kilimo (ASDP), Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Miradi ya Maji (WSDP), Miradi ya Afya (HBF), Miradi ya Malaria, Ukimwi na Kifua kikuu (Global Funds) na mingineyo inayotekelezwa katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Pia nimefanya ukaguzi wa ufanisi na kutoa Ripoti 6, na pia nimefanya kaguzi maalum 16 katika Halmashauri 6, Wizara 4 na Mashirika ya Umma 6. Hivyo kwa ujumla wake Ofisi imefanya jumla ya kaguzi 983 kwa mwaka 2012/2013.

## Hati za Ukaguzi

3. Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2013, nimetoa jumla ya Hati za Ukaguzi 961 (bila kujumlisha kaguzi maalum 16 na za ufanisi 6). Kati ya hati hizo, Hati zinazoridhisha ni 816 (85%), Hati zenye shaka ni 131 (13.6%), Hati zisizoridhisha 8 (0.8%) na Hati mbaya 6 (0.6%). Pamoja na kwamba kuna jumla ya hati mbaya sita na hati zisizoridhisha nane kwa taasisi zote nilizokagua kwa mwaka huu, mwelekeo wa Hati za ukaguzi, kwa ujumla unaonyesha kuimarika kwa utendaji wa Serikali katika kusimamia makusanyo ya mapato na matumizi ya rasilimali za umma ikilinganishwa na miaka iliyopita.

4. Misingi ya aina ya Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka huu imefafanuliwa kwa kina katika ripoti husika ambazo ni: Ripoti ya Serikali Kuu na Taasisi zilizopo chini yake, Ripoti ya Serikali za Mitaa, Ripoti ya Mashirika ya Umma na Ripoti ya Miradi ya wafadhili. Nakala ya ripoti hizo mtapewa na pia zimeshawekwa kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (www.nao.go.tz).

5. Ufuatao ni mchanganuo unaoonyesha Idadi ya Hati zilizotolewa kwa mwaka 2012/13 katika tarakimu na asilimia:

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Hati nilizozitoa Mwaka 2012/2013**

| **Na.** | **Taasisi zilizokaguliwa** | **Idadi ya Taasisi zilizokaguliwa** | **Aina ya hati za ukaguzi** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Hati zinazoridhisha** | **Hati yenye shaka** | **Hati isiyoridhisha** | **Hati mbaya** |
| **1** | Wizara, Idara na Taasisi zake | 117 | 85 (73%) | 30 (26%) | 1 (0.5%) | 1 (0.5%) |
| **2** | Halmashauri | 140 | 112 (80%) | 27 (19%) | 1 (1%) | 0 |
| **3** | Mashirika ya Umma | 93 | 92 (99%) | 1 (1%) | 0 | 0 |
| **4** | Miradi ya Wafadhili | 611 | 527 (86%) | 73 (12%) | 6 (1%) | 5 (1%) |
| **Jumla** | | **961** | **816(85%)** | **131(13.6%)** | **8[1] (0.8%)** | **6[2] (0.6%)** |

6. Hati zenye shaka kwa upande wa Serikali Kuu zimeongezeka kutoka hati 5 kwa mwaka 2011/12 hadi Hati 30 kwa mwaka 2012/13, ikiwa imeongezeka mara tano zaidi. Ongezeko hili, limesababishwa na mambo yafuatayo:

i. Uandaaji wa Hesabu kwa kufuata mfumo mpya wa viwango vya kimataifa vya Uhasibu yaani **IPSAS 'Accrual'** unaotambua madeni na mali za kudumu zinazomilikiwa na Serikali kitu ambacho kwa Serikali kuu kilikuwa hakifanyiki miaka ya nyuma, kwani mfumo wa **IPSAS Cash** ulikuwa hauhitaji kufanya hivyo.

[1] **Hati zisizoridhisha:** Ubalozi wa Muscat, Jiji la Mwanza, Manispaa ya Sumbawanga (ASDP), Wilaya ya Sumbawanga (HBF), Wilaya ya Mpanda (HBF), Wilaya ya Chunya (WSDP), Manispaa ya Sumbawanga (WSDP) na Jiji la Mwanza (WSDP).

[2] **Hati Mbaya:** Hesabu Jumuifu za Taifa, Wilaya ya Mbozi (ASDP), Wilaya ya Mbozi (HBF), Wilaya ya Singida (TASAF), Wilaya ya Bariadi (TASAF) na Wilaya ya Mbozi (WSDP)

ii. Changamoto nyingi zilijitokeza wakati wa uandaaji wa Hesabu hizo na hivyo wahusika kushindwa kukidhi kikamilifu matakwa ya mfumo huo wa kiuhasibu zikiwepo changamoto za utumiaji wa mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS-Epicor).

iii. Kutojumuishwa kwa Hesabu za Halmashauri na Mashirika ya Umma kwenye Hesabu Jumuifu za Taifa ilisababisha Hesabu hizo kupata hati mbaya.

7. Kwa upande wa Halmashauri, Hati zinazoridhisha zimeongezeka kutoka asilimia 78 hadi 80 kwa mwaka uliopita. Wakati upande wa Mashirika ya Umma, Hati zinazoridhisha zimeongezeka kutoka asilimia 90 hadi 99. Wakati huohuo, Hati zinazoridhisha kwa upande wa Ripoti za Wafadhili zimeongezeka kutoka asilimia 81 hadi asilimia 86.

**Utekelezaji wa Mapendekezo Niliyoyatoa Miaka Iliyopita**

8. Katika kupitia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi niliyoyatoa miaka iliyopita, mapendekezo hayo yamegawanywa katika mafungu matatu, yaani ya muda mfupi, ya muda wa kati na ya muda mrefu. Jumla ya mapendekezo 102 yalitolewa kwa serikali kwa kupitia taarifa zangu za miaka iliyopita. Kwa ujumla mapendekezo 22 sawa na asilimia 22.5 ya mapendekezo yaliyotolewa yalifanyiwa kazi kikamilifu na mapendekezo 57 yanaendelea kufanyiwa kazi sawa na asilimia 55.5 na mapendekezo 23 sawa na asilimia 23 utekelezaji wake upo katika hatua za awali kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 2: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo niliyoyatoa mwaka 2011/2012**

| Na. | Ripoti | Jumla ya Mapendekezo yaliyotolewa | Mapendekezo yaliyotekelezwa | Mapendekezo ambayo utekelezaji wake unaendelea | Mapendekezo ambayo utekelezaji wake upo katika hatua za awali |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Serikali Kuu | 28 | 5 | 23 | 0 |
| **2** | Serikali za Mitaa | 33 | 2 | 17 | 14 |
| **3** | Mashirika ya Umma | 41 | 15 | 17 | 9 |
| **Jumla** | | **102** | **22** | **57** | **23** |

**Mambo yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa Serikali Kuu na Taasisi zilizoko chini yake**

**Utekelezaji wa Mfumo wa viwango vya kimataifa vya uandaaji wa Hesabu kwa msingi usio wa Fedha taslimu *(IPSAS Accrual)***

9. Kuanzia tarehe 1 Julai 2012, Serikali Kuu ilianza rasmi utumiaji wa mfumo mpya wa viwango vya Kimataifa wa kuandaa Hesabu wa ***IPSAS accrual*** na kuachana na mfumo wa ***IPSAS Cash*** ambao ulikuwa na mapungufu mengi. Baadhi ya faida za Mfumo huu mpya ni kuiwezesha serikali kuandaa Hesabu Jumuifu zinazounganisha Hesabu za Serikali Kuu, Hesabu za Serikali za Mitaa na Hesabu za Mashirika ya Umma. Pia kuiwezesha Serikali kujua idadi ya mali zote ilizonazo ikijumuisha majengo, Mitambo, Magari, samani na wadeni wake. Pia mfumo huu utasaidia Serikali kujua serikali inadaiwa kiasi gani na nani anayedai.

10. Pamoja na mambo mazuri yatokanayo na utumiaji wa mfumo huu, utekelezaji wake umekuwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:

a) Bajeti kuendelea kuandaliwa katika mfumo wa ***'Cash basis'*** wakati hesabu zinaandaliwa katika mfumo wa ***IPSAS accrual***, hali hii inasababisha kutofautiana kwa taarifa.
b) Sheria kutoboreshwa ili ziendane na msingi wa uandaaji wa Hesabu kwa kutumia mfumo wa *IPSAs accrual*,
c) kukosekana kwa miongozo iliyoandaliwa kuwawezesha wahusika wakiwemo Maafisa Masuuli kuandaa hesabu zinazokidhi viwango vinavyotakiwa na mfumo huu mpya, na
d) Kukosekana kwa Kamati ya kitaifa inayoshughulika na usimamizi na utekelezaji wa mfumo huu mpya ambao unahitaji Taasisi na Idara mbalimbali kuhusishwa katika kipindi cha miaka mitano ya kukamilisha utekelezaji wa mfumo wenyewe.

**11. Ningependa kusisitiza kuwa katika Ukaguzi nilioufanya, nilibaini mapungufu katika utekelezaji wa mpango *(Road map*) wa mfumo huu wa**

***IPSAS accrual*** **ulioanza 1 Julai 2012. Ingawa utekelezaji huu umetoa kipindi cha mpito cha hadi miaka mitano kukamilisha mambo mbalimbali. Ningependa kusisitiza Serikali iongeze kasi katika kuondoa mapungufu yaliyojitokeza ili hatimae kuwa na mfumo dhabiti wa** ***IPSAS Accrual*****. Baadhi ya mapungufu hayo ni kama vile kukosekana kwa Hati za umiliki wa mali za Serikali, kuna kazi ambazo hazijakamilishwa kwa muda uliopangwa (mfano, uthaminishaji wa mali za Serikali), kukosekana kwa uratibu (*coordination*) na kutokuwepo kwa miongozo ya uandaaji wa Hesabu kwa kutumia mfumo huu kama vile '*Accounting Policies'* na mingineyo.**

**Usimamizi wa Bajeti**

12. Bajeti ni chombo muhimu sana katika kusimamia ukusanyaji na matumizi ya fedha, pia ni chombo kinachosaidia Serikali katika usimamizi na mwelekeo wa kifedha na kiuchumi. Katika ukaguzi wangu nimebaini mapungufu yanayohitaji maboresho katika utekelezaji/usimamizi wa bajeti ya Serikali kama vile:

(a) Uwekaji wa ukomo wa bajeti ***(budget ceiling)*** usio na uhalisia wala kuangalia umuhimu wa shughuli au huduma zinazotolewa na Taasisi za Serikali kwa mfano Idara ya Magereza.

(b) Maandalizi ya bajeti kutokuzingatia taarifa za miaka iliyopita kama vile utambuzi wa madeni na hivyo kusababisha bajeti kutotekelezeka,

(c) Nidhamu hafifu katika matumizi kwa kukiuka matumizi ya vifungu mbalimbali katika bajeti kama ilivyoidhinishwa na Bunge,

(d) Kutokuzingatia taarifa za tathmini zinazoandaliwa kila mwezi zinazoonyesha mwelekeo wa matumizi kulingana na vipaumbele vilivyowekwa (***performance reports***),

(e) Fedha za maendeleo kutotolewa kama ilivyoidhinishwa na Bunge au kutolewa mwishoni mwa mwaka ambapo kunakuwa hakuna muda wa kuzitumia.

13. Ukaguzi uliofanyika katika bajeti umegundua pia kuna mambo mengine ambayo kwa mtazamo wa kikaguzi yanafanya utekelezaji wa bajeti usiwe wa ufanisi kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 3: Mapungufu yanayohusiana na bajeti (Serikali Kuu na Serikali za Mitaa)**

| Na. | Upungufu uliojitokeza | Halmashauri (Bilioni) | Asilimia (%) | Serikali Kuu (Bilioni) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Fedha za maendeleo ambazo hazikutolewa kulingana na bajeti | 253.31 | 38 | 977.94 | 23 |
| **2** | Fedha za matumizi ya kawaida ambazo hazikutolewa | 275.40 | 13 | 315.46 | 4 |
| **3** | Fedha zilizotumika kinyume na bajeti iliyoidhinishwa | 0.74 | 0.02 | 15.79 | 0.12 |
| **4** | Fedha za maendeleo ambazo hazikutumika | 243.68 | 36 | 44.43 | 1 |
| **5** | Fedha za matumizi ya kawaida ambazo hazikutumika | 146.33 | 5 | 35.14 | 0.41 |

Miradi ambayo haikukamilika kwa mwaka husika kwa Halmashauri ilikuwa na thamani ya Sh. Billion 497. Kati ya hizo asilimia 38 ya bajeti haikutolewa na Hazina (unreleases of development funds), na asilimia 36 ya fedha zilizotolewa hazikutumika (unspent). Kutotumika kwa fedha kumechangiwa na ucheleweshwaji wa utoaji fedha wa Hazina kwenda Halmashauri, mchakato mrefu wa Manunuzi na Halmashauri kushidwa kutimiza masharti ya wafadhili.

Kwa upande wa Serikali Kuu miradi yenye thamani ya Sh. Billioni 1,022.4 haikukamilika. Kati ya hizo asilimia 23 ya bajeti, fedha hizo hazikutolewa na Hazina, na asilimia 1 ya fedha zilizotolewa hazikutumika.

**Deni la Taifa na Misamaha ya Kodi**

14. Deni la Taifa ni eneo ambalo limekuwa na changamoto kwa muda mrefu sasa, hasa katika upatikanaji wa taarifa sahihi zinazohusu ukuaji wa deni hilo na manufaa yake kwa nchi. Kazi ya Ukaguzi wa Deni la Taifa na Misamaha ya Kodi bado inaendelea na nitatoa taarifa kamili hivi karibuni.

15. Hata hivyo, katika ripoti nilizowasilisha leo, nimegusia baadhi ya mambo yanayohusu deni la Taifa na misamaha ya kodi kama ifuatavyo:

16. Kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2013 hali halisi ya Deni la Taifa lilifikia kiasi cha Sh.trilioni 21.20, ongezeko la Sh. trilioni 4.23 (sawa na asilimia 25) ikilinganishwa na kiasi cha Sh. trilioni 16.98 mwaka 2011/2012. Deni hili linajumuisha deni la ndani na deni la nje.

17. Hali halisi ya deni la ndani ilifikia kiasi cha Sh. trilioni 5.78 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2013, ikiwa ni ongezeko la Sh. trilioni 1.23 (sawa na asilimia 27) kutoka kiasi cha Sh. trilioni 4.55 mwaka 2011/2012.

18. Kwa upande wa deni la nje limeongezeka na kufikia kiasi cha Sh. trilioni 15.43 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2013, ongezeko la Sh. trilioni 3 (ikiwa ni asilimia 24) kutoka Sh. trilioni 12.43 mwaka 2011/2012.

19. Ongezeko hili lilisababishwa na mikopo kutoka kwa mabenki na wafadhili wa nje kwa ajili ya kusaidia miradi mikubwa ya maendeleo kama vile uboreshaji wa miundombinu katika nyanja za usafirishaji, maji safi, mkongo wa mawasiliano wa taifa na bomba la gesi.

**20. Ni maoni yangu kwamba, pamoja na Deni la Taifa kuongezeka, uchumi wa nchi nao umekuwa na kuimarika kutokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali kama nilivyoainisha hapo juu.**

**Misamaha ya Kodi**

21. Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatoa misamaha ya kodi kwa walengwa mbalimbali kwa lengo la kukuza biashara na kwa sababu za kibinadamu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo. Taarifa za misamaha ya kodi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2013 zimeonyesha kuwa kiasi cha Sh. trilioni 1.52 kilitolewa kama misamaha ya kodi.

22. Mwenendo umeonyesha kuwa misamaha ya kodi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2013 imepungua kutoka Sh. trilioni 1.81 mwaka 2011/2012 hadi Sh. trilioni 1.52

mwaka 2012/2013, upungufu wa Sh. bilioni 290.60 sawa na asilimia 16 hivyo napenda kuipongeza Serikali kwa hatua ilizozichukua za kupunguza misamaha ya kodi kwa kiasi hicho. Ukilinganisha na bajeti nzima ya Serikali kwa mwaka 2012/2013, misamaha ya kodi inafikia asilimia 10 ya bajeti yote.

23. Hivyo ni imani yangu kuwa, kupitia kazi ninayoendelea nayo ya kuchambua misamaha hii, itawezesha kutoa mwanga wa mianya ambayo inaweza ikazibwa zaidi ili kuiwezesha Serikali kuongeza mapato yanayokusanywa.

**Ukaguzi wa Magereza**

24. Idara ya Magereza ni idara muhimu inayoshughulikia maisha ya watanzania walioko magerezani. Kwa kawaida, Magereza yana kazi tatu za msingi,

(a)usalama na udhibiti wa wahalifu,

(b) kuwaadhibu wahalifu na

(c) kuwabadilisha wahalifu kuwa raia wema.

25. Kwa sasa kuna magereza 122 nchini yanayojumuisha magereza ya wanaume, wanawake na watoto. Uwezo wa Magereza yote 122 kwa sasa yanatoa huduma kwa wafungwa wapatao 45,000 wakati uwezo wa magereza haya ni wafungwa 22,669 tu ikiwa ni zaidi kwa 99%. Hali hii imeongeza ugumu wa kudhibiti na kufuatilia haki za wafungwa kwenye magereza yenye msongamano mkubwa kiasi hicho.

26. Ukaguzi wangu katika Idara ya Magereza ulibaini mambo yafuatayo:

a) Ufinyu wa Bajeti. Kwa mwaka 2012/13 Idara ya Magereza ilibajeti kiasi cha Shs. Bilioni 131.5 kwa matumizi ya kawaida na Shs. Bilioni 51.60 kwa miradi ya maendeleo. Kutokana na ufinyu wa bajeti, Idara ya Magereza walipewa bajeti yenye ukomo wa Shs. Bilioni 51.4 kwa matumizi ya kawaida na Shs. Bilioni 1.3

kwa shughuli za maendeleo. Baadhi ya maeneo yaliyoathirika kutokana na ukomo wa bajeti ni kama ifuatavyo:

| **Maelezo** | **Mahitaji halisi** | **Bajeti iliyoidhinishwa** | **Tofauti** | **Upungufu Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| | **A** | **B** | **C=B-A** | |
| **Chakula cha wafungwa** | 32.4 bilioni | 8 bilioni | 24.4 bilioni | 75% |
| **Mavazi ya wafungwa** | 1.6 bilioni | 0.5 bilioni | 1.1 bilioni | 68% |
| **Sare za Askari** | 3.7 bilioni | 0.35 bilioni | 3.4 bilioni | 91% |

**Usimamizi wa Rasilimali Watu**

27. Rasilimali watu katika uendeshaji wa Serikali ni eneo muhimu ambalo Serikali inatakiwa kulisamimia kwa ufanisi ili kuhakikisha kunaleta tija katika kuwatumikia wananchi.

28. Katika ukaguzi wangu, imebainika kuwa upande wa Serikali Kuu na Ofisi za Sekretarieti za Mikoa, kwa kuchukulia sampuli 28 zilizofanyiwa ukaguzi, jumla ya watumishi wanaohitajika ni 22,160, wakati waliopo ni 9,536 tu. Hivyo kufanya upungufu wa watumishi 12,624 idadi ambayo ni sawa na **asilimia 57**. Kwa upande wa Serikali za Mitaa, katika sampuli ya Halmashauri 73, kati ya watumishi 183,095 wanaohitajika katika Halmashauri hizo, idadi iliyopo ni watumishi 143,111 tu. Hivyo kusababisha upungufu wa watumishi 39,984 sawa na **asilimia 22**.

**29. Katika maeneo mengi, sababu zilizotolewa ni kucheleweshwa kwa vibali vya kuajiri kutoka Utumishi na sababu nyingine ni uhaba wa fedha ili kuweza**

**kujaza nafasi zilizo wazi. Hivyo, ili kuleta ufanisi, napendekeza kuendelea kusisitiza ushauri nilioyoutoa katika ripoti zilizopita kuwa;**

i. Serikali ifanye ukaguzi wa rasilimali watu (manpower audit) kwa nchi nzima ili iweze kujua mahitaji halisi ya watumishi.
ii. Kuboresha utaratibu uliopo wa utoaji wa vibali vya ajira na
iii. Uharakishaji wa mchakato mzima wa utoaji wa vibali vya ajira nchini.

**Mishahara iliyolipwa kwa Watumishi Walioacha Kazi au Kufariki**

30. Ukaguzi wangu pia umebaini kuwa mishahara ya watumishi walioacha kazi, waliofariki, waliostaafu, wameendelea kulipwa mishahara kupitia katika akaunti zao. Vilevile, fedha za makato ya mishahara ya Wafanyakazi hao zimeendelea kupelekwa kwenye taasisi husika kama vile Bima ya Afya ya Taifa, Mamlaka ya Mapato, Mifuko ya Jamii, n.k. Hali hii imesababishwa na watumishi hawa kuchelewa kutolewa katika orodha ya mishahara ya watumishi wote. Jumla ya kiasi kilicholipwa kwa sampuli ya watumishi wa aina hii ni Sh. Bilioni 1.62 na makato yake ni Sh.milioni 497. Hali hii bado inaendelea licha ya kuwa Serikali imewekeza kwenye mfumo wa LAWSON kama njia mojawapo ya kudhibiti hali hiyo.

**Pamoja na kuwepo na mfumo wa Lawson kuna haja kwa Serikali kuimarisha udhibiti wa ndani wa ajira na malipo ya mishaara kwa watumishi wa umma.**

**Vilevile kuna umuhimu wa Serikali kudai fedha zilizolipwa vizivyoalali kutoka kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mamka ya Mapato na mabenki.**

**Usimamizi wa Manunuzi**

31. Mapungufu katika manunuzi yanazidi kujitokeza pamoja na mapendekezo niliyoyatoa katika ripoti zangu zilizopita. Yafuatayo ni mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi wangu wa Mwaka 2012/13 katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa:

| Na. | Mapungufu |
|---|---|
| 1 | Manunuzi yaliyofanyika bila ushindanishi wa bei |
| 2 | Manunuzi ya mali ambazo hazitumiki |
| 3 | Malipo zaidi ya kiwango kilichotajwa kwenye mkataba |
| 4 | Manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa manunuzi |
| 5 | Manunuzi yaliyofanyika bila kibali cha Bodi ya zabuni |
| 6 | Manunuzi yaliyolipwa kwa njia ya masurufu |
| 7 | Vifaa vilivyonunuliwa pasipo kuingizwa katika leja |
| 8 | Manunuzi kutoka kwa wafanyabiashara wasioidhinishwa na Bodi za Zabuni |
| 9 | Vifaa ambavyo havikupokelewa ingawa malipo yalifanyika |
| 10 | Taarifa muhimu za mikataba zilikuwa zinakosekana |

**Usimamizi wa Mali**

32. Kulikuwa na mapungufu katika utunzaji na usimamizi wa mali za kudumu na za muda mfupi za Serikali. Mifumo ya usimamizi wa ndani (***Controls***) iliyopo haitoi uthibitisho wa usahihi wa idadi ya mali za kudumu zilizopo na thamani yake halisi.

Mapungufu hayo ni kama vile:

a) kukosekana kwa nyaraka zinazothibitisha umiliki wa mali zilizopo,
b) kutokuwepo kwa daftari linaloonyesha mali za serikali kwa usahihi
c) Mali zilizochakaa kuendelea kuonekana katika orodha ya mali zilizopo
d) mali zilizopo kutofanyiwa tathmini kwa muda mrefu
e) kujumuisha mali katika thamani isiyo sahihi
f) Baadhi ya mali zitokanazo na misaada kutojumuishwa kwenye vitabu.

**Ukaguzi wa Vyama vya Siasa**

33. Mwaka huu wa Ukaguzi umekuwa ni mara ya kwanza, kwa Ofisi yangu kukagua Hesabu za Vyama vya Siasa zoezi ambalo linaendelea. Hii inatokana na kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992. Nitakapokamiliza zoezi hili nitakua katika nafasi ya kutoa ripoti ya kina zaidi juu ya ukaguzi wa Vyama vya Siasa hapa nchini.

34. Hata hivyo, katika ripoti nilizowasilisha leo, nimeonyesha baadhi ya mambo ambayo yamejitokeza katika ukaguzi wa awali wa vyama kumi (10) kati ya vyama (21) vyenye usajili wa kudumu vilivyowasilisha hesabu zao kwa ajili ya ukaguzi:

a) Vyama vya siasa 11 kati ya 21 vyenye usajili wa kudumu havikuwasilisha taarifa za hesabu za mwaka kwa mujibu wa Kifungu cha 14(1)(b) (i) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992.
b) Taarifa za hesabu zilizowasilishwa na vyama hivyo hazikufuata misingi ya uhasibu na mfumo wa utoaji taarifa za fedha wa kimataifa.
c) Hesabu za Vyama vya Siasa saba (7) vilivyokaguliwa hazionyeshi mali za kudumu na za muda mfupi zinazomilikiwa na vyama hivyo kinyume na kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992.
d) Vyama vya Siasa vinne (4) vilivyokaguliwa havina akaunti ya benki kinyume na kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992.
e) Tulibaini kuwa hakuna chama cha siasa hadi sasa kilichowasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa tamko la mali zote zinazomilikiwa na chama husika kinyume na kifungu cha 14 (1) (b)(ii) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992.

**35. Ili kuboresha utoaji wa taarifa, uwasilishwaji na ulinganifu wa utendaji wa vyama vya siasa, napendekeza kuwa vyama viandae taarifa za hesabu kwa mujibu wa viwango vya kihasibu vya kimataifa. Msajili wa vyama vya siasa akishirikiana na Mhasibu Mkuu wa Serikali watoe mwongozo wa aina ya mfumo na muundo wa taarifa za fedha utakaotumiwa na vyama vya siasa.**

**Changamoto**

36. Kwa mujibu wa kifungu cha 14(1)(i) cha sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992 inanihitaji nikague vyama vya siasa. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi nimekutana na changamoto katika ukaguzi wa fedha ambazo si za umma. Kwa mujibu wa wajibu wangu kikatiba kwenye ibara 143(2)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, 1977 natakiwa kukagua fedha na rasilimali za umma. Katika hali hiyo kuna utata kama kifungu hicho cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinakidhi haja ya mimi kufanya ukaguzi wa fedha za vyama ambazo siyo za umma.

**Masuala mengine yanayohusu Serikali za Mitaa**

**Usimamizi katika Ukusanyaji wa Mapato kutoka vyanzo vya ndani**

37. Ukaguzi wangu umebaini kuwepo kwa mapungufu katika ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vya ndani. Kwa upande wa Serikali za Mitaa ukusanyaji wa mapato ya ndani unaathiriwa na:

1) Usimamiaji usioridhisha wa mikataba ya mawakala wa kukusanya mapato ambapo kiasi cha Sh. bilioni 6.71 hazikupelekwa katika Halmashauri husika,
2) Makusanyo ambayo hayakupelekwa benki kiasi cha Sh. milioni 585.50,
3) Kutofanyika kwa upembuzi yakinifu ili kuweza kubaini vyanzo vipya vya mapato pamoja na kutokuweka kwa viwango sahihi vinavyotakiwa kuletwa na wakala wa ukusanyaji mapato,
4) Utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu ambao unapelekea vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato kupotea.

**38. Naendelea kuishauri Serikali kuliangalia upya eneo hili la ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa lengo la kuboresha na kukuza ukusanyaji wa mapato hayo ili kuziongezea Halmashauri hizo uwezo wa kujitegemea katika matumizi ya kawaida.**

**Mambo yaliyojitokeza kwenye Ukaguzi wa Mashirika ya Umma**

39. TANESCO ililipa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 1.71 kwa kuchelewa kumruhusu mzabuni kuanza kazi ya mradi wa njia ya umeme katika maeneo ya Kurasini na Mbagala kutokana na kuchelewa kufanya upembuzi yakinifu wa mradi huo. Pia, nilibaini kuwa gharama za mshauri wa mradi ziliongezeka kutoka Euro milioni 1.70 hadi Euro milioni 2.55 sawa na ongezeko la Euro 848,910 bila idhini ya Bodi ya Zabuni.

40. Ukaguzi wa usimamizi wa mikataba ya TANESCO ulibaini kuwa Shirika hili lililipa gharama za ziada za jumla ya shilingi bilioni 9.5 kwa kampuni za SEMCO Maritime AS na

Rolls Royce Maritime AS kutokana na kucheleweshwa kwa mradi kwa miezi kumi kulikopelekea kufanyika upya kwa kufanya upembuzi yakinifu.

41. Mwaka 2006, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilinunua mita nane kwa gharama za Sh. 2.46 kutoka kampuni ya ***FMC Energy System*** kwa ajili ya kudhibiti shehena ya mafuta yanayoingizwa nchini. Hata hivyo, mita hizo zimetelekezwa kwa kipindi kirefu baada ya Wakala wa Vipimo kusitisha matumizi yake hivyo kukosekana kwa thamani ya fedha ya matumizi hayo.

42. Katika kipindi cha mwezi Agosti na mwezi Septemba, 2012, magari 11 yaliyonunuliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa ajili ya Bodi ya Biashara (TanTrade) yalisajiliwa kwa namba binafsi. Ilithibitika kuwa magari hayo hayakupokelewa na TanTrade baada ya usajili. Pia ilibainika kuwa Mamlaka haikujulishwa yalikopelekwa magari hayo hadi tarehe ya uandaaji wa ripoti hii.

43. Kulingana na taarifa za Msajili wa Hazina mwaka 2008 Serikali ilikuwa inamiliki kwa asilimia 100 taasisi ya PRIDE Tanzania. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi ya PRIDE Tanzania ilitolewa kwenye daftari la Msajili wa Hazina bila maelezo ya kina. Pia, Benki ya Azania inamilikiwa kwa zaidi ya asilimia 91 na mifuko ya Pensheni ambayo ni Mashirika ya Umma, vilevile Banki ya Maendeleo ya Wanawake Tanzania inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 99.

**Taasisi zote tatu nilizozitaja hazijawahi kuwasilisha taarifa za Hesabu kwangu kwa ajili ya ukaguzi.**

**Mambo yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

44. Katika ukaguzi wangu wa miradi ya Maendeleo inayojumuisha miradi ya ASDP, TASAF, WSDP, na HBF, nimebaini mapungufu yafuatayo:

a) Miradi pamoja na programu za maendeleo haisimamiwi ipasavyo na kuwepo kwa upungufu wa wataalam wa sekta husika, na pia kutokuwa na taarifa za kuridhisha juu ya utekelezaji wa miradi hiyo na namna fedha ilivyotumika kukamilisha lengo lililokusudiwa.

b) Mapungufu mengine katika ukaguzi wa miradi ni kama vile;
   - miradi iliyokamilika kutokutumika Sh. milioni 393.49,
   - miradi ambayo haikukamilika kwa wakati Sh. bilioni 1.58,
   - matumizi yasiyokuwa na viambatisho Sh. bilioni 4.55,

- o kukosekana kwa hati za malipo (*Payment vouchers*) Sh. bilioni 1.63.

45. Vilevile lengo kuu la kutoa fedha za miradi ni kuzitumia katika kuwaletea wananchi maendeleo. Hata hivyo, katika ukaguzi wangu nimebaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 275.60 hakikutumika katika mwaka uliopita. Pia, kwa mwaka huu, kiasi cha fedha Sh. bilioni 329.95 (sawa na asilimia 37) kati ya Sh. bilioni 892.31 zilizokuwepo hazikutumika katika mwaka 2012/2013 kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

| Miradi/Sh. | Fedha ambazo hazikutumika kipindi kilichopita (Bilioni) | Fedha iliyopokelewa (Bilioni) | Kiasi kilichokuwepo kwa ajili ya utekelezaji (Bilioni) | Matumizi (Bilioni) | Kiasi ambacho hakikutumika (Bilioni) | Bakaa katika % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **TASAF** | 6.12 | 23.04 | 29.17 | 26.23 | 2.93 | 10.04 |
| **ASDP** | 33.61 | 22.45 | 56.06 | 41.28 | 14.78 | 26.36 |
| **WSDP** | 223.07 | 404.14 | 627.21 | 348.89 | 278.32 | 44.37 |
| **HBF** | 12.80 | 167.07 | 179.88 | 145.96 | 33.92 | 18.86 |
| **Jumla** | **275.60** | **616.71** | **892.31** | **562.36** | **329.95** | **36.89** |

Hii inaonyesha kuwa kuna mapungufu katika kusimamia malengo yaliyokusudiwa.

## Ukaguzi wa Ufanisi

46. Kwa upande wa Ukaguzi wa Ufanisi, kwa kipindi kinachoishia Machi 2014, nimetoa ripoti sita kama ifuatavyo:

## A. Udhibiti wa Gharama Katika Manunuzi ya Umma

47. Ukaguzi huu ulilenga kuchunguza ili kubaini kama Wizara, Taasisi za Serikali pamoja na Serikali za Mitaa zina utaratibu madhubuti unaoweza kudhibiti gharama za manunuzi ya umma katika maeneo yao. Ukaguzi huu ulijikita katika manunuzi ya tiketi za ndege kwa watumishi wa umma pamoja na ujenzi wa majengo katika Serikali za Mitaa. Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

a) Mipango, bajeti na makadirio ya gharama hayakuwa na uhalisia.
b) Vyombo vya udhibiti kutoshughulikia masuala ya udhibiti wa gharama katika manunuzi ya umma ipasavyo.
c) Wakandarasi na watoa huduma hawasimamiwi vya kutosha na malipo kwa makandarasi na watoa huduma kufanyika bila ya ukaguzi makini wa kazi

iliyofanyika au huduma iliyotolewa. Hali hii inaweza kufafanuliwa kupitia mfano ufuatao:

**Tofauti ya Bei Zinazolipwa na Bei Zilizoko Kwenye Mikataba**

48. Mawakala wa usafiri wa anga walitakiwa kutoza gharama ya huduma kama ilivyo katika Mikataba iliyoandaliwa na GPSA. Hata hivyo, mawakala wamekuwa wakitoza gharama za huduma kwa viwango ambavyo ni zaidi ya vile vilivyoko kwenye mikataba na GPSA. Kwa mfano, sampuli ya LPO 42 iliyochukuliwa ikiwakilisha safari 468 za maofisa wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilibainisha kuwa bei ya gharama ya huduma ilitozwa zaidi ya kiwango kilichokubaliwa. Matokeo yake Wizara ililipa Sh. milioni 114.8 badala ya Sh. milioni 41.9 hivyo kupelekea malipo ya ziada ya Sh. milioni 72.9 ambayo ni karibu mara tatu ya gharama zilizotakiwa kulipwa.

**Mawakala Kuchagua Bei za Juu Zaidi**

49. Mapitio ya mikataba ya manunuzi yalionesha hapakuwa na kipengele ambacho kingeweza kumfanya wakala kuchagua bei za chini. Matokeo yake, mawakala wamekuwa wakitoza bei za juu kwa zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya kima cha chini japokuwa kulikuwa na fursa ya kupata tiketi zilezile kwa bei za chini zaidi.

50. Kwenye sampuli ya tiketi 32 za usafiri wa ndani, kulikuwepo na fursa za mawakala kuchagua bei kati ya Sh. 60,000 na Sh. 470,000. Hata hivyo bei halisi zilizochukuliwa zilikuwa kati ya Sh. 109,000 mpaka Sh. 360,000. Matokeo yake taasisi ililipa Sh. 7.5 milioni ambapo kulikuwa na uwezekano wa kulipa chini zaidi kufikia Sh. 4.1 milioni na kuokoa kiasi cha Sh. milioni 3.4. Kwa wastani, nusu ya tiketi za safari za ndani ziligharimu kiasi cha Sh. 100,000 zaidi ya kiwango cha chini cha nauli wakati wa kufanya manunuzi (booking).

51. Vilevile, kwenye sampuli ya tiketi 45 za safari za nje, kulikuwepo fursa ambayo ingemwezesha wakala kuchagua bei nafuu. Matokeo yake wizara ililipa kiasi cha Sh. 611.9

milioni ingawa wangeweza kulipa kiasi cha chini kufikia Sh. 366.6 milioni na kuokoa ongezeko la kiasi cha Sh. 162.3 milioni.

**Kwa wastani, nusu ya tiketi zilizonunuliwa kwa safari za nje ziligharimu Sh. 2 milioni kila moja zaidi ya kiwango cha chini kilichokuwepo wakati wa kufanya manunuzi.**

### Kutowekwa Wazi kwa Taarifa Muhimu kwenye Tiketi za Ndege

52. Mapitio ya tiketi yalionesha kuwa asilimia 12.5 ya sampuli ya tiketi 32 kwa safari za ndani zilionesha kiasi cha nauli. Sampuli ya tiketi 72 kwa safari za kimataifa ilionesha kuwa ni asilimia 11 tu ya tiketi zilizokuwa na taarifa muhimu ikiwemo nauli na mchanganuo wa kodi. Tiketi zilizobaki hazikuonesha taarifa muhimu kama vile gharama za huduma, kodi, kiasi cha nauli na mahesabu ya kukokotoa nauli. Taarifa hizi ni muhimu na hutakiwa kuwepo kwenye tiketi kwani ni sehemu ya mkataba kati ya mnunuzi na mnunuaji wa huduma na zinatakiwa kuwekwa bayana.

### Kutokuwepo kwa Bei Elekezi na Makadirio yasiyo Sahihi kwenye Miradi ya Ujenzi

53. Asilimia 47 ya miradi iliyokaguliwa haikuwemo kwenye mipango ya manunuzi ya mwaka. Asilimia 16 ya miradi haikuwa na makadirio ya mhandisi. Asilimia 45 ya miradi yote haikuwa na bajeti ingawa ilitekelezwa. Baadhi ya Halmashauri ziliweka fungu kwenye bajeti kwa ajili ya ujenzi wa madarasa bila kuonesha/kuorodhesha shule zilizohusika na idadi ya madarasa yaliyotarajiwa kujengwa.

## B. Utambuzi na Utoaji wa Huduma kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi

54. Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hawakuwa na mifumo ya udhibiti kwa upande wa utambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na uchambuaji wa mahitaji yao. Kati ya watoto wahitaji wapatao 894,515

waliotambuliwa, ni asilimia 44 tu ya watoto hao waliweza kupatiwa kiwango cha chini cha mahitaji yao halisi na waliobaki hawakupatiwa mahitaji yao sawasawa. Hivyo, huduma zilitolewa hazikuwa na manufaa tosha kwao.

55. Sababu zilizopelekea Serikali ishindwe kutoa huduma za msingi kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi ni pamoja na:

a) kutokuwepo kwa mifumo endelevu na inayokidhi viwango vya utoaji wa huduma kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi,
b) Uhaba wa Maafisa Ustawi wa Jamii waliopatiwa mafunzo ya kusimamia utoaji wa huduma za msingi kwa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi. Uhaba wa Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi za mikoa ni asilimia 12 wakati katika Halmashauri za Wilaya ni asilimia 80,
c) Kutokuwepo kwa uratibu na utoaji taarifa katika ngazi zote za Serikali katika kusimamia shughuli za kuwahudumia watoto wanaoishi katika Mazingira Hatarishi,
d) Uhaba wa fedha za kuwahudumia watoto wanaoishi katika Mazingira Hatarishi. Halmashauri za Wilaya zilitenga kati ya Shilingi 239 mpaka Sh. 11,614 kwa matumizi ya kila mtoto kwa mwaka. Hiki ni kiasi kidogo sana na haiwezi kukidhi mahitaji ya hata wiki moja ya mtoto huyo.

## C. Ukaguzi wa Bidhaa Zinazotoka Nje ya Tanzania

56. Ukaguzi ulilenga kufanya tathmini kama Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linafanya ukaguzi wa kutosha na wa mara kwa mara wa bidhaa zinazoingia nchini katika kupunguza bidhaa zisizo na ubora katika soko la Tanzania. Nilibaini kuwa ukaguzi uliofanywa na Shirika la Viwango Tanzania haukuweza kuzuia ipasavyo uingiaji wa bidhaa zisizo na ubora hapa nchini. Hii ilitokana na sababu zifuatazo:

a) Kukosekana kwa mipango na malengo ya kaguzi zilizofanywa. Vilevile, kaguzi hizo zilifanywa pasipo kuzingatia viashiria hatarishi (***risk factors).*** Bidhaa zote zilipewa

kipaumbele sawa wakati wa ukaguzi licha ya kwamba athari za bidhaa zinatofautiana.

b) Shughuli za Shirika la Viwango nchini zipo katika maeneo machache ya nchi ambayo ni bandari na mipaka 6 tu kati ya 32 iliyopo kisheria hapa nchini. Hivyo, bidhaa zilizoingizwa kupitia mipaka 26 ambayo haikuwa na Wakaguzi wa ubora kutoka TBS, hazikuweza kukaguliwa.

c) Kukosekana kwa uratibu na ushirikiano baina ya mamlaka husika katika ukaguzi wa bidhaa. Mamlaka hizo ni pamoja na Mamlaka ya Mapato (TRA), Mamlaka ya Chakula na Madawa (TFDA), Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Mambo ya Ndani n.k.

**D. Ukaguzi wa Vyakula**

57. Ukaguzi ulilenga kutathmini kama Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) inatimiza dhamira yake ya kulinda ubora wa chakula nchini. Ukaguzi ulijikita katika mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya ukaguzi wa ubora wa chakula katika viwanda vinavyosindika chakula na katika mipaka inayotumika kuingiza chakula nchini. Nilibaini kuwa, ukaguzi wa usalama wa chakula katika viwanda vya kusindika chakula na bandari za kuingiza bidhaa nchini hautoshelezi, hali iliyosababishwa na:

a) Kukosekana kwa mipango na malengo ya kaguzi zilizofanywa. Vilevile, ukaguzi huo ulifanywa pasipo kuzingatia viashiria hatarishi. Viwanda vyote vilipewa kipaumbele sawa wakati wa ukaguzi licha ya kwamba vihatarishi baina ya vyakula na taratibu za uzalishaji wa vyakula hivyo hutofautiana;

b) Ukaguzi makini haukufanyika kwa bidhaa za chakula ambazo kiasili zinaweza kuwa hatarishi. Hili lilichangiwa na mosi, mizigo midogo midogo ya chakula kupita mipakani bila ya kukaguliwa, kwa mfano katika kipindi cha miaka miwili moja ya

mipaka nchini ilipitisha jumla ya kilogramu 25,200 za bidhaa aina ya blue band bila ya kukaguliwa; pili kuruhusiwa kwa bidhaa ambazo hazijasajiliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania kuingia nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2012/13, ni asilimia 43 ya bidhaa za chakula zilizoingizwa nchini zilikuwa zimekaguliwa na sehemu iliyobaki, yaani asilimia 57 zilikuwa ni zile ambazo hazijasajiliwa na hivyo hazikutakiwa kuingia nchini;

c) Kutokuchukua hatua dhidi ya vitendo vya ukiukwaji wa Sheria na taratibu za usalama wa chakula nchini.

## E. Uwindaji wa Wanyamapori

58. Ukaguzi ulilenga kuchunguza kama Wizara ya Maliasili na Utalii inasimamia na kufuatilia ipasavyo shughuli za uwindaji wa wanyamapori na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na wanyamapori katika mapori ya akiba (***Game Reserves***) na mapori tengefu (***Game Controlled Areas***). Ukaguzi ulibaini udhaifu ufuatao:

a) Doria hazifuatiliwi na kufanyiwa tathmini ipasavyo,
b) Udhaifu katika usimamiaji wa sheria zinazotumika kutoa adhabu kwa wahalifu wanaouhusika na vitendo viovu vya kuangamiza wanyama pori
c) Wizara kutofanya tathmini ya kina kwa makampuni ya uwindaji kwa kipindi cha kuanzia 2009 hadi 2012.
d) Kutokuwa na utaratibu sahihi wa kusimamia ukusanyaji wa mapato. Kwa mfano, ukaguzi ulibaini kuwa makampuni 36 hayakulipia ushuru wa utalii wa picha hivyo kuisababishia Serikali hasara ya mapato ya Sh.bilioni 2.7. Hii ilitokana na kutokuwa na utaratibu sahihi katika kusimamia utalii wa picha.

**F. Usimamizi wa Taka zitokanazo na Huduma za Afya**

59. Ukaguzi huu ulilenga kuchunguza kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ( TAMISEMI) zinahakikisha kwamba taka hatarishi zitokanazo na tiba zinasimamiwa vizuri ili kulinda afya ya jamii na mazingira. Kupitia ukaguzi uliofanyika, nilibaini kuwa:

a) Utenganishi wa taka zitokanazo na huduma za afya haufanyiki ipasavyo, na mitambo ya kuchoma taka imechakaa hivyo taka hazichomwi vizuri na kuwa majivu kama inavyotakiwa (kwa mfano, katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya, taka zinazofanyiwa utenganishi ni chini ya asilimia 50 ya zile zilizozalishwa).
b) Mamlaka za Serikali za Mitaa hazisimamii na kufuatilia vya kutosha utendaji wa shughuli za usimamizi wa taka katika vituo vya huduma za afya. Mfumo uliopo wa kupeleka taarifa kutoka ngazi za chini hadi Wizarani hautoi nafasi kwa habari za taka zitokanazo na huduma ya afya. Hivyo ni vigumu kupima maendeleo na kutambua maeneo dhaifu yanayohitaji kuboreshwa.

**Mapendekezo ya Jumla katika Ripoti za Ufanisi**

60. Ninapendekeza yafuatayo:

**61. Serikali na Taasisi zake zote zianzishe Kamati za Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba ambazo zitakuwa zikipitia na kuhakiki mikataba ya manunuzi kabla ya kusainiwa na Serikali na Taasisi za Umma kama ilivyo kwenye kifungu Na 60 (4) cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 kwa Serikali za Mitaa.**

**62. Serikali ifanye utafiti yakinifu na kuangalia njia za kuboresha utendaji wa Mamlaka ya Chakula na Dawa, Bodi mbalimbali za Chakula na Shirika la Viwango nchini ili kuboresha utendaji wao kwa nia ya kuondoa muingiliano usio wa msingi. Pendekezo hili linatolewa baada ya kuona kuwa kuna muingiliano wa majukumu ya Taasisi hizi mbili.**

**Kwa sasa TBS, Bodi za mazao na TFDA wote wanafanya kazi za kufanana za kukagua usalama wa bidhaa zinazoingizwa nchini. Taasisi hizi zinawajibika kwa wizara mbali mbali hivyo, zinaleta ugumu wa kuratibu shughuli hii muhimu kwa Taifa. Muingiliano huu hauna tija kwa taifa, hivyo, kuna umuhimu kwa serikali kuangalia njia bora za kuoanisha shughuli za Taasisi hizi.**

**63. Pia ninapendekeza kuwepo na Sera ya Usalama wa Chakula nchini (*Food Safety Policy*) ambayo itaelezea majukumu ya kila mhusika kwani kwa sasa ni vigumu kupata ripoti ya hali ya usalama wa chakula nchini kwa kuwa mfumo uliopo hivi sasa unahusisha wadau wengi ambao hawajaratibiwa ipasavyo.**

**Mapendekezo ya Jumla kwa Serikali**

64. Kifungu Na. 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 kinanitaka kutoa mapendekezo yangu Serikalini kwa jambo lolote linaloweza kuongeza mapato, kupunguza upotevu wa rasilimali za serikali na kupunguza matumizi yasiyokuwa na tija. Hivyo, kwa msingi wa kifungu hiki napenda kutoa mapendekezo yafuatayo:

**65. Kutokana na kupanda kwa gharama za kupanga ofisi za Serikali, kuna umuhimu kwa Serikali kuwekeza katika majengo yake yenyewe. Ukaguzi wa 2012/13 ulibaini ofisi 14 za Serikali zililipa jumla ya Sh. Bilioni 7.9 kama kodi ya pango kwa mwaka. Ninaishauri Serikali kuwa na mpango endelevu wa kujenga majengo kwa ajili ya ofisi zake.**

**66. Uongozi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (MFAIC) uone uwezekano wa kuanzisha mfuko katika bajeti yake kwa ajili ya kufanya shughuli za diplomasia ya kiuchumi na kukuza vivutio vya utalii, kwa kuzingatia kwamba hii ni kazi muhimu kwa uchumi wa nchi.**

**67. Kuanzisha kamati ya kitaifa ya kuratibu utekelezaji wa IPSAS ambayo itashirikisha wataalam na wadau mbalimbali ambao watakuwa wasimamizi wa**

**jukumu hili kwa miaka minne iliyobaki ili kuhakikisha kila hatua inatekelezwa kwa umakini na kwa wakati.**

**68. Uwepo wa miji ya kisasa unaenda sambamba na miundombinu ya taa za barabarani *(street lights*). Manufaa ya uwepo wa taa za barabarani mijini ni pamoja na kuimarisha usalama wa raia na mali zao na kuwezesha shughuli za kiuchumi kufanyika mchana na usiku na pia kuongeza mandhari ya miji. Hali hii ni tofauti kabisa katika miji yetu. Hivyo tunashauri uanzishwaji wa Mradi wa Taa za Barabarani. OWM-TAMISEMI iitishe mkutano wa kitaalam utakaowahusisha TANESCO, Halmashauri, Mabenki na wadau wengine kujadili njia sahihi ya kuanzisha mradi wa taa za Barabarani katika miji yote nchini. Hii ni pamoja na kumtumia mshauri atakayeainisha pamoja na mambo mengine:**

**a) aina ya umeme unaopaswa kutumika kwa bei nafuu**
**b) jinsi Halmashauri zitakavyopata fedha za kugharamia mradi huo,**
**c) Uanzishwaji wa mradi huo kwa mafanikio.**

**69. Mapendekezo Yanayohusu Idara ya Magereza**

**Kutokana na changamoto inayoikabili Idara ya Magereza ya Tanzania ninapendekeza yafuatayo kwa Serikali na kwa Idara yenyewe:**

**a) Mahakama ya Tanzania iharakishe kutoa maamuzi juu ya kesi zilizopo kwani kwa sasa kuna idadi kubwa ya mahabusu katika magereza ambao wanasubiri kesi zao kusikilizwa na haki kutolewa. Hii itawezekana tu pale Serikali itakapoiwezesha Mahakama kuwa na uwezo wa kufanya kazi zake za kikatiba ipasavyo. Hii ni pamoja na kuipatia Mahakama fedha, nyenzo na watumishi wenye sifa na idadi inayoendana na majukumu yake.**

b) **Ili kupunguza msongamano katika Magereza na gharama za kuwahudumia wafungwa Mahakama inashauriwa kutoa adhabu mbadala kwa makosa madogo madogo.**

c) **Kwa makusudi kabisa Serikali ione umuhimu wa kubuni mradi kabambe wa upanuzi wa miundo mbinu ya Magereza ikiwa ni pamoja na kujenga magereza mapya na kukarabati yaliyopo**.

d) **Kutokana na wingi wa wafungwa na mahabusu waliopo kwenye magereza yetu kuna umuhimu wa serikali kutenga fedha za kutosha kulisha, kuvalisha na kutibu wafungwa hii ikiwa ni moja ya haki yao ya msingi.**

e) **Inashauriwa kuwa Idara ya Magereza ipime ardhi iliyonayo kwa madhumuni ya kupata hati miliki ili iweze kuitumia kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuingia ubia wa shughuli za uzalishaji/biashara na sekta binafsi (PPP).**

f) **Idara ya Magereza inashauriwa kukiimarisha kitengo chake cha kibiashara (*Prisons Corporation Sole*) ili kichangie katika kuongeza mapato ya Idara hii.**

**70. Mali na Fedha Zisizokuwa na Mwenyewe (*Unclaimed assets)***

**Ukaguzi umebaini kuwa katika Taasisi za Fedha na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini zimekuwa na fedha ambazo zinakaa muda mrefu bila kuchukuliwa na wenyewe kutokana na sababu mbali mbali kama vile kufariki dunia, makato ya kisheria kwa wafanyakazi walioachishwa kazi au kustaafu ambapo Hazina huendelea kupeleka makato hayo katika mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Amana ambazo zimetelekezwa na wenyewe kutokana na uchache wake, fedha za mirathi, fedha haramu na gawio zisizochukuliwa. Katika nchi mbali mbali**

**kuna sheria zinazozitaka Taasisi zinazojikuta zina fedha kama hizo kutakiwa kuzipeleka katika mfuko maalum unaotunzwa na Hazina. Fedha hizo huwa zinatunzwa kwenye mfuko huo kwa kipindi maalum kabla hazijatumiwa kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Endapo mwenye fedha hizo atajitokeza na vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa madai yake, mfuko utamrejeshea kiasi anachostahili kulipwa.**

**Kutokana na uchumi wa nchi kukua na Watanzania wengi zaidi kuamua kutumia Taasisi za fedha ikiwa ni pamoja na kushiriki katika Soko la Hisa na Mitaji, ninaishauri serikali iandae muswada wa Sheria ya kushughulikia fedha na mali za aina hii.**

**Ndugu Waandishi wa Habari, haya ni baadhi tu ya mambo yaliyojitokeza katika taarifa zangu kumi zilizowasilishwa leo Bungeni. Ni imani yangu kwamba wadau wote watapata nafasi ya kuzisoma kwa kina na kuzitumia.**

**Kama nilivyotangulia kusema awali, ripoti hizi zinapatikana pia katika tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo ni www.nao.go.tz zikiwa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.**

**Kwa kumalizia napenda kwa dhati kabisa kuishukuru Serikali yetu tukufu kwa mchango wake mkubwa katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Vile vile napenda kulishukuru Bunge letu tukufu kupitia kamati zake tatu za usimamizi ambazo ni PAC, LAAC na Kamati ya Bajeti. Kadhalika, ninapenda kuwatambua na kuwashukuru wadau mbalimbali waliochangia kufanikisha utekelezaji wa majukumu yangu kikatiba wakiwemo wafadhili (USAID, SNAO, WB, SIDA, GIZ, DFID, CNAO, DANIDA, FINIDA na wengineo), vyombo vya habari pamoja na taasisi zisizo za kiserikali ambazo zinafanya kazi kubwa ya kuelimisha wananchi kuhusu taarifa za ukaguzi.**

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**

**Ludovick S.L Utouh**

**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**7 Mei, 2014**